

**SONGWE REGION CO-OPERATIVE UNION LIMITED (SORECU)**

**MWALIKO WA ZABUNI**

1. Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Songwe (SORECU LTD) kimetenga fedha mahsus kwa ajili ya ununuzi wa Mizani za Kidigitali na utoaji wa huduma za Usafirishaji wa Mazao na uendeshaji wa Maghala katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026. Sehemu ya fedha zilizotengwa zitatumika kulipia mahitaji ya ununuzi huo halali chini ya mkataba maalum ambao utatolewa kupitia zabuni hizi. Hivyo unaalikwa kuchukua kabrasha la tenda, kulijaza na kurudisha kulingana na muda uliotolewa likionesha bei kama ilivyoelekezwa katika kabrasha hilo.
2. Lifuatalo ni jedwali lioneshalo mchanganuo wa zabuni zitakazoshindanishwa kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026;

Na.	NAMBA YA ZABUNI	JINA LA ZABUNI
1	SORECU/2025-2026/G/10	UNUNUZI WA MIZANI ZA KIDIGITALI
2	SORECU/2025-2026/G/09	UNUNUZI WA VIFUNGASHIO VYA MAZAO (UFUTA)
3	SORECU/2025-2026/NC/03	HUDUMA YA USAFIRISHAJI MAZAO
4	SORECU/2025-2026/NC/02	HUDUMA YA UENDESHAJI WA MAGHALA

3. Tenda zitashindanishwa kwa washindani (wazabuni) wa ndani ya nchi tu kwa kufuata utaratibu wa sheria za ununuzi. Wazabuni ambao wanawiwa na kupendelea kushindana wanaweza kupata taarifa za ziada na kununua makabrasha ya tenda katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, S.L.P 148, Mbozi katika Mkoa wa Songwe kuanzia tarehe 20/03/2025 mpaka tarehe 29/03/2025 kuanzia saa mbili (02:00) kamili asubuhi hadi saa kumi (10:00) kamili jioni. Sherehe ya ufunguzi wa tenda itafanyika mara tu baada ya kukamilisha ukusanyaji wa zabuni siku na saa hiyo iliyopangwa.
4. Baada ya kukusanya zabuni katika ofisi ya mkuu wa kitengo cha Ununuzi, kutakuwa na ghamraza za kununua kabrasha la zabuni husika, na kila zabuni itagharimu kiasi cha shilingi za kitanzania laki nane (Tsh 800,000/=) tu, fedha hii hairudishwi(Non-refundable). Kiasi hiki kiwekwe katika akaunti ya SORECU LTD namba 0150427373001. katika benki ya CRDB PLC.
5. Zabuni zote ziwekwe katika bahasha tatu ndogo (A4) zikiwemo, bahasha moja ni asili (original) na nyingine mbili ni nakala (copy) za zabuni hiyo. Kisha bahasha zote tatu ziwekwe katika bahasha kubwa (A3) moja na juu ya bahasha hiyo iandikwe kama ifuatavyo;

**Katibu wa Tenda,  
Songwe Region Co-operative Union Limited,  
S.L.P.148,  
Mbozi - Songwe.**

- 
6. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa kwa njia nyingine tofauti na anuani tajwa hapo juu au zilizowasilishwa katika muundo usiokubalika hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yaliyo sababisha.
  7. Wazabuni wote au wawakilishi wao watatakiwa kuhuduria siku ya sherehe ya ufunguzi wa tenda **terehe 09/04/2025 saa sita (06:00) kamili mchana mara tu baada ya kukamilisha** kupokea zabuni katika ukumbi wa mikutano wa SORECU LTD.
  8. Wazabuni wote ni lazima wawe wamesajiliwa wakiwa wameambatanisha leseni halali za biashara, hati halali ya usajili wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT), cheti chenye namba ya mlipa kodi (TIN), orodha ya mikataba iliyotekelizwa kipindi cha karibuni pamoja na maelekezo mengine yapatikanayo katika kabrasha la tenda.
  9. Kwa mawasiliano zaidi tafadhali tupigie kwa namba + **255 769 461 391**.